**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOKETI TAREHE 20/12/2021 KATIKA OFISI YA MANUNUZI (HPMU):**

**WAJUMBE WA BODI YA ZABUNI WALIOHUDHURIA:-**

1. Natujwa N. Mellau - Mwenyekiti
2. Peter M. Lebalwa - Katibu
3. Msifwaki N. Haule - Mjumbe
4. Mary M. Kayowa - Mjumbe
5. Sia Ngao - Mjumbe

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA**

1. Maajabu A. Kanyemka - Mjumbe
2. Cotrida Komba - Mwalikwa

**WAJUMBE WAALIKWA**

1. Eng. Omary Sima - Mhandisi Ujenzi
2. Dr. Phillipina Phillipo - DMO
3. Dr. Thabit R. Mdai - MOI

**SEKRETARIET (PMU):-**

1. Ramadhani A. Mpanda

**AGENDA ZA KIKAO**

1. Kufungua Kikao.
2. Kuthibitisha na kupitisha agenda za kikao.
3. Kupitia nyaraka za zabuni na kuidhinisha Wakandarasi watakaopewa nyaraka za zabuni kwa kazi ya kuchimba kisima katika kijiji cha Mingo kata ya Lubungo na kijiji cha Magali kata ya Melela.
4. Kupitia na kuidhinisha nyaraka za zabuni na orodha ya wakandarasi kazi ya ujenzi wa jengo la dharura (EMD) na nyumba ya watumishi.
5. Mengineyo
6. Kufunga Kikao.

**KUMB.NA.HW. 081/BZ/2020/2021/03/01: KUFUNGUA KIKAO.**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 03:11 asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe kuchangia hoja zitakazowasilishwa katika kikao.

**KUMB.NA.HW. 081/BZ/2020/2021/03/02: KUTHIBITISHA NA KUPITISHA AGENDA ZA KIKAO.**

Katibu wa bodi ya zabuni alisoma agenda za kikao na kisha wajumbe waliridhia na kupitisha agenda sita (06).

**KUMB.NA.HW. 081/BZ/2020/2021/03/03: KUPITIA NYARAKA ZA ZABUNI NA KUIDHINISHA WAKANDARASI WATAKAOPEWA NYARAKA ZA KAZI YA KUCHIMBA VISIMA KATIKA VIJIJI VYA MINGO NA MAGALI:**

Katibu wa bodi ya zabuni aliwasilisha agenda hii kama ifutavyo;



Scanned with CamScanner

Kitengo cha manunuzi kilipokea maombi ya kuchimba visima vya maji katika vijiji vya Mingo na Magali kutoka idara ya Kilimo na Umwagiliaji.

Hivyo katibu aliomba ridhaa ya bodi ya zabuni kupitia nyaraka za zabuni na kuidhinisha orodha ya wakandarasi watakaopewa nyaraka hizi. Aidha pia aliomba idhini ya kutumia njia ya manunuzi ya 'Restricted Tendering Method (Shopping) ambapo 'una-shortlist' wakandarasi baadhi wenye sifa kulingana na aina na ukubwa wa zabuni.

Bodi ya zabuni ilijadili taarifa iliyowasilishwa na katibu wa bodi ya zabuni. Baadhi ya maswali yalikosa majibu ya kina yaliyojitosheleza, ikiwa ni pamoja na 'malengo mahususi ya visima, kiasi tengefu na chanzo cha fedha kwa ajili ya kazi hizi, na maelekezo ya utekelezaji wa miradi hii kutoka ngazi ya Wizara kama ipo. Pia kwa nini iwasilishwe kama agenda ya dharura?

Bodi ya zabuni haikuridhia na kutoidhinisha mchakato wa ununuzi wa wakandarasi kwa ajili ya kazi za uchimbaji visima vijiji vya Mingo na Magali.

Aidha bodi ya zabuni iliagiza, idara ya kilimo kushirikiana na katibu wa bodi ya zabuni iandae taarifa ya kina inayojitosheleza ikielezea mradi kwa kina, ikiwa ni pamoja na chanzo cha fedha, malengo mahususi ya mradi, na maelekezo ya Wizara katika utekelezaji wa mradi kwa ujumla. Pia bodi ilielekeza kuwa agenda hii iwasilishwe kwenye kikao cha kawaida na sio dharura.

**KUMB.NA.HW. 081/BZ/2020/2021/03/04: KUIDHINISHA NYARAKA ZA ZABUNI NA ORODHA YA WAKANDARASI KAZI YA UJENZI WA JENGO LA DHARURA (EMD) NA NYUMBA YA WATUMISHI.**

Katibu wa bodi ya zabuni aliwasilisha agenda hii kama ifutavyo;

Kitengo cha manunuzi kilipokea maombi ya ujenzi wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma ya dharura (EMD) na nyumba ya watumishi katika Hospitali ya Wilaya ya Mvomero kutoka idara ya Afya ikieleza kuwa;-

Ofisi ya Rais – TAMISEMI imepokea fedha kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za Afya ya Msingi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia mpango maalum wa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 kwa kutumia fedha za mkopo wa mashariti nafuu kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF).

Moja ya miradi itakayotekelezwa kwa fedha hizo ni ujenzi wa majengo ya kutolea huduma ya dharura (EMD), majengo ya kuhudumia wagonjwa mahututi (ICU), wodi ya magonjwa ya mlipuko (Treatment Centre) na nyumba ya watumishi.



Scanned with CamScanner

Kati ya miradi hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero imepata miradi miwili ambayo ni ujenzi wa jengo ya kutolea huduma ya dharura (EMD) na nyumba moja ya watumishi; yenye thamani ya jumla Tsh. 390,000,000.00.

Kwa mujibu wa kanuni ya manunuzi 185 na 163 (3) (4) ya mwaka 2013 ikisomwa pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2016, bodi ya zabuni shariti iidhinishe i. njia ya manunuzi, ii. orodha ya wazabuni watakaoshindanishwa, iii. Tangazo la zabuni na iv. Nyaraka za zabuni.

Hivyo kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W), katibu wa bodi ya zabuni aliomba wajumbe wapitie na kuidhinisha;

i. **Njia ya manunuzi: -** National Restricted Tendering Method: kwa sababu muda wa kutangaza gazetini kitaifa inahitaji zaidi ya siku 14, wakati hii ni siku 7.

ii. **Orodha ya wazabuni** watakaoshindanishwa ambo ni;

**a) Jengo la dharura (emergency building).**

1. PACHA CONSTRUCTION COMPANY LIMITED,
   P.O BOX 5230,
   MOROGORO.
   **BUILDING CLASS 2**
2. NGOGO ENGINEERING LTD,
   P. O. BOX 552,
   MAKAMBAKO
   **BUILDING CLASS 3**
3. M.C.M GLASS AND ALUMINIUM WORKS LIMITED,
   P.O. BOX 16598,
   DA ES SALAAM
   **BUILDING CLASS 4**
4. DEO CONSTRUCTION COMPANY LIMITED,
   P.O. BOX 40312,
   DA ES SALAAM
   **BUILDING CLASS 4**
5. PRINCE GENERAL INVESTMENT LIMITED,
   P. O. BOX 9934,
   DAR ES SALAAM
   **BUILDING CLASS 3**

**b) Nyumba ya watumishi (Staff house)**

1. DIOCESE OF MOROGORO (ANGLICAN CHURCH) TECHNICAL SUPPORT CO. LTD,
   P.O BOX 320,
   MOROGORO.



Scanned with CamScanner

**BUILDING CLASS 7.**

2. UNIT (T) LIMITED,
   P. O. BOX 70513,
   DAR ES SALAAM
   **BUILDING CLASS 6**
3. BEMFRANK (T) LTD,
   P. O. BOX 292,
   IRINGA.
   **BUILDING CLASS 6**
4. S. K BUILDING AND CIVIL ENGINEERING WORKS LTD,
   P. O. BOX 24629
   DAR ES SALAAM
   **BUILDING CLASS 7**
5. LUMOCONS CO. LTD,
   P. O. BOX 10679,
   DAR ES SALAAM.
   **BUILDNG CLASS 5**
6. MMETO CONSTRUCTION COMPANY LIMITED,
   P. O. BOX 2735,
   DAR ES SALAAM
   **BUILDING CLASS 5**
7. NKEMWA TANZANIA LTD,
   P. O. BOX 209,
   SONGEA.
   **BUILDING CLASS 5**

iii. **Tangazo la zabuni:** - Tangazo limeambatanishwa

iv. **Nyaraka za zabuni:** - Nyaraka zimeambatanishwa.

Katibu wa bodi ya zabuni alieleza kuwa, kutokana na uhitaji wa utaalam maalum (specialised works) kwenye majengo ya EMD na ICU, Wizara iliagiza, wakandarasi wa miradi hii wasiwe chini ya daraja la nne (4); yaani class four. Hivyo wazabuni waliopendekezwa kuidhinishwa na bodi ya zabuni kwa mradi wa ujenzi wa jengo la EMD ni kuanzia class four kwenda juu kulingana na maagizo ya ofisi ya Rais TAMISEMI.

Aidha Mganga Mfawidhi, Mganga Mkuu (W) na Mhandisi Ujenzi (W) walitoa maelezo ya miradi kwa kina ikiwa ni pamoja na maelekezo mbalimbali ya Serikali Kuu kuhusu utekelezaji ma miradi hii.

Wajumbe wa bodi ya zabuni waliuliza maswali ya uelewa na kutolewa ufafanuzi kutoka pande husika.



Scanned with CamScanner

Baada ya mawasilisho na majadiliano, bodi ya zabuni iliridhia maombi na mapendekezo ya katibu wa bodi ya zabuni na kuidhinsha i. njia ya manunuzi, ii. orodha ya wazabuni watakaoshindanishwa, iii. Tangazo la zabuni na iv. Nyaraka za zabuni kama zilivyowasilishwa na katibu wa bodi ya zabuni.

Hivyo bodi ya zabuni iliridhia utekelezaji wa miradi hii uendelee kama ulivyokusudiwa kwa kuzingatia muda kulingana na maagizo ya serikali kuu, pia kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za manunuzi.

**KUMB.NA.HW. 081/BZ/2020/2021/03/05: KUFUNGA KIKAO.**
Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao kisha kufunga kikao saa 05:53 asubuhi.

**"UMETHIBITISHWA"**

| | |
|---|---|
| ................................................ | ................................................ |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |
| ....31/12/2021.... | ....31/12/2021.... |
| **TAREHE** | **TAREHE** |



Scanned with CamScanner

YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 20/12/2021

| NA | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 1. | Taarifa ya kina inayoelezea malengo mahususi ya visima, kiasi tengefu na chanzo cha fedha kwa ajili ya kazi hizi, na maelekezo ya utekelezaji wa miradi hii kutoka ngazi ya Wizara kama ipo. | Userdepartment/Katibu wa bodi ya zabuni | Limetekelezwa: taarifa imewasilishwa kama agenda. |
| 2. | Agenda ya visima vya maji iwasilishwe kwenye kikao cha kawaida na sio kikao cha dharura. | Katibu wa bodi ya zabuni | Limetekelezwa: Agenda imeingia kwenye kikao cha kawaida na sio kama dharura. |
| 3. | Kuendelea na mchakato wa manunuzi kwa miradi ya ujenzi wa jengo la EMD na nyumba ya watumishi. | Katibu wa bodi ya zabuni | Mchakato wa manunuzi umefanyika na unaendelea hadi utakapokoma baada ya kusainiwa mikataba. |



Scanned with CamScanner